## KENYA CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION (K.C.S.E)

KISWAHILI

FASIHI 102/3

Muda: saa 2½

Machi 2018

Jina ________________________ Nambari ya Mtahiniwa _______

Sahihi ___________________ Tarehe ____________

**Maagizo:**

*a) Andika Jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
*b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
*c) Jibu maswali **manne** pekee*
*d) Swali la **kwanza** ni la **lazima***
*e) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwa kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani: Riwaya, Tamthilia, Fasihi simulizi na Hadithi Fupi*
*f) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja***
*g) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**Kwa matumizi ya Mtahini pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1. | 20 | |
| 2. | 20 | |
| 3. | 20 | |
| 4. | 20 | |
| 5. | 20 | |
| 6. | 20 | |
| 7. | 20 | |
| 8. | 20 | |

## SEHEMU A: SHAIRI

**Swali la lazima**

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

**Wanaume ni wanyama**

Nakumbuka vyema sana, sisahau siku ile
Nilipoitwa na nina, akanipa ya kivyele
Mwanangu umsichana, nakuasa usikile
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

Kuwa umevunja ungo, ni hali ya maumbile
Bora uwapo na bongo, anasa uzikimbile
Ukijitia maringo, utatungwa mimba mbele
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

Ngawa waje na manoti, "Nakupenda" wakwambile
Wakuvalie makoti, usiwaachie mbele,
Hata wapige magoti, wambile mna kelele
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

Ngono ni tendo la suna, Amina sikimbilile
Wala miguu halina, kwamba lingekukimbile
Muhimu kwako Amina, kwanza uthamini shule
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

Kuzurura mitaani, si tabia njema ile
Unapotoka nyumbani, fululiza hadi shule
Si kwenda vichochoroni, kuwaona kina wale
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

Uwe mwana msikizi, yano uyazingatile
Mengine kuhusu penzi, mwanangu taonywa shule
Kama mameyo mzazi, nimekuonya kimbele
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

Wakaja kina Hamadi, mwana wa Mzee sule
Kwangu wakapiga hodi, hata mkuu wa shule
Ila nikajitahidi, kukwepa mitego ile
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

Na kuna huyo Karisa, mwanafunzi kule shule
Akawa hunipapasa, name vile vile
Mwishowe ikatupasa, tugawe tunda tule
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

Nani akachovya uto, wa asali tamu vile
Na kisha aape kuto, kula asali milele
Kuwa ni mjamzito, wamenifukuza shule
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

Karisa yu vilevile, angali yuwaenda shule
Na mie kitumbo mbele, ninajikuna upele
Yameshatimia yale, niloonywa siku ile
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

**Maswali**

a) Shairi hili lina dhamira gani? alama 2
b) Eleza aina ya shairi hili alama 2
c) Onyesha jinsi mshairi aliweza kutumia idhini ya kishairi katika utunzi wake alama 4
d) Tambua nafsi neni katika shairi. Thibitisha alama 2
e) Andika ubeti wa sita kwa lugha ya riwaya alama 4
f) Taja mambo matatu ya nafsi neni kama ushauri kwa mnenewa alama 3
g) Kwa kutoa mifano, fafanua tamathali tatu alizotumia mshairi alama 3

## **SEHEMU B:- RIWAYA**

Ken walibora – Kidagaa kimemwozea

Jibu swali 2 au 3

2.**:** “Hatuwezi kuwa binadamu endapo hatuwaoni walemavu kama wenzetu. Tutakuwa tumelemaa ulemavu mbaya zaidi kuliko ulemavu.”

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili alama 4

b) Eleza kwa tafsili ulemavu katika riwaya alama 12

c) Taja na ueleze maudhui mawili yanayoendelezwa na msemaji katika dondoo hili alama 4

3. Viongozi wanachangia kuzorata kwa maendeleo katika jamii. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa mujibu wa riwaya ya kidagaa kimemwozea. alama 20

## **SEHEMU C: TAMTHILIA**

Pauline kea – Kigogo

Jibu swali la 4 au la 5

4. “Ukichinja watoto wa wenzio usiulizwe?”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili alama 4

b) Taja tamathali mbili za lugha zinazojitokeza katika dondoo alama 4

c) Ni jambo gani lililopelekea msemaji kusema hayo? alama 4

d) Onyesha namna watoto wa wengine walivyochinjwa alama 8

5. “Utawala wa majoka katika jimbo la sagamoyo umejaa Sumu ya nyoka.” Jadili usemi huo kwa kurejelea tamthilia ya kigogo alama 20

## **SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI**

Jibu swali la 6 au 7

6. a) Eleza maana ya tanzu zifuatazo za fasihi simulizi

i) Miviga

ii) Mighani

iii) Visasili

iv) Ngano alama 8

b) Taja sifa nne za mtambaji katika Fasihi simulizi alama 4

c) Eleza maana ya ngomezi alama 2

d) Toa sifa za ngomezi alama 5

7.a) Fafanua mambo matano yanayochangia kubadilika kwa Fasihi simulizi
alama 10

b) Eleza dhima ya methali kama kipera cha fasihi simulizi alama 10

**SEHEMU E:-HADITHI FUPI**

Alifa Chokocho na Dumu Kayanda:-Tumbo lisiloshiba na hadithi nyingine

8. "Unafikiria mambo mabaya… unafikiria mambo maovu!"

a) Weka dondoo hili katika muktadha ukirejelea 'shogake Dada ana Ndevu'
alama 4

b) Ni mambo yapi aliyofikiriwa mzungumzaji? Alama 2

c) Eleza sifa za mzungumzaji na ufafanue umuhimu wake alama 14

**Fasihi ya Kiswahili 102/3**
**Mwongozo**
**Shairi**

a) Shairi limelenga kuwafunua macho vijana hasa wasichana kuhusu hatari zilizopo katika ujana
lina lenga kuwatahadhirisha wasichana dhidi ya hadaa kutoka kwa wanaume – watawapachika mimba na kuwaacha

b) Tarbia – lina mishororo mine – katika kila ubeti
kutaja – 1, maelezo 1 = alama 2

c) i) Inkisari – ngawa – ingawa
taonywa – utaonywa

ii) Tabdila – ukimbile – ukimbie
usikile – usikie

iii) Kuboronga/kufinyanga/kubananga
- Ngono – ni tendo la suna, Amina sikimbilie
  Amina sikimbile ngono si tabia tendo la suna
- Kuzurura mitaani, si tabia njema ile
  Ile tabia ya kuzurura mitaani si njema 2 x 2 =alama 4

d) Mama yake mshauriwa alama 1
"Kama mamayo mzazi, nakuonya ukimbilie alama 1

e) Uwe mwana anayesikia/msikivu wa kuzingatia yafuatayo
mambo kuhusu mapenzi utaonywa shuleni lakini nikiwa mama yako mzazi
ninakuonya kimbele ujihadhari na wanaume kwa sababu ni wanyama alama 4

f) Akimbie anasa
asijitie maringo
asitungwe mimba
asifanye ngono
asizurure mitaani
akitoka nyumbani afululize

asitembee vichochori
ajiepushe na wanaume 3 x 1 = alama 3

g) Jazanda/istiari – wanaume ni wanyama
Tashihisi/uhaishaji – wala miguu halina kwamba lingekukimbile
Taswira – kuzurura mitaani 3 x 1= alama 3

**<u>Riwaya – keri walibora</u>**

2.a) Ni mawazo ya mwandishi
Kupitia kwa majisifu, katika kumbukizi ya majisifu na kubadilika kwa kumwona imani anawalea vyema wanawe walemavu – lakini bado mlevi 4 x 1=alama 4

b) i) Ulemavu wa maungo/viungo k.m watoto wa majisifu
ii) -Msichana katika matwana
iii) Ulemavu wa akili/wendawazimu – matuko weye
iv) -mashaka kuwehuka
v) Ulemavu wa kiuchumi – maskini katika sokomoko
vi) Ulemavu wa kitaaluma – majisifu kushindwa kuwasilisha
vii) mhadhara katika chuo kikuu
viii) Ulemavu wa kimaadili –mtemi Nasaba Bora kuwa mfisadi
mkware, mpyaro
ix) -Fao kumringa msichana wa shule
x) Ulemavu wa kiafya – Chwechwe Makweche
xii) - watoto, waliokuwa na DJ, walikuwa na utupia mlo
xiii) Ulemavu wa kimaendeleo – kujenga zahanati badala ya hospitali

xiv) Mwalimu majisifu kuiba mswada wa Amani
xv) Mtemi kutumia lugha ya kingereza kuhutubia wanasokomoko wasiolewe chochote
xvi) Wauguzi kukataa kumtibu uhuru na kudai kuwa ni sikukuu ya uhuru
xvii) Mtemi kuishi katika kasri chafu bila kunadhifisha na kuwafuta wafanyikazi
10x1=10alama

c) Mabadiliko majisifu alibadilika na kukoma kuwadharau walemavu
haki za watoto wa majisifu/
utu/wema
uwajibikaji – majisifu anatekeleza wajibu kulea watoto 4 x 1 = alama 4

3.
i) Wanashiriki wizi wa mali ya umma k.v. Mtemi kunyakua mashamba

ii) Wanafeli kuwahakikishia wananchi usalama k.v. mama Imani
iii) Wanaendeleza upujufu wa maadili mf Mtemi Nasaba
iv) Wanatoa ajira duni kwa mshahara duni mf Amani kwa Mtemi
v) Wanawachapa raia, Nasaba kumchapa Amani
vi) Wanakwepa kazi na kushiriki na ulevi. Mwalimu majisifu
vii) Fao anashiriki mapenzi na mwanafunzi wake na kumringa
viii) Balozi kuendeleza propaganda isiyofaa uongozi wa sokomoko
ix) Majisifu kutowajali wanawe walemavu kwa kukosa kuwapa elimu maalum ya walemavu
x) Askari kuwapiga raia bila sababu. Mamake Imani
xi) Nasaba Bora anakataa kunadhifisha mazingira yake
xii) Anawafuta wafanyikazi bila sababu
xiii) Wazazi wa fao wanahugumu hadhi ya mitihani ya kitaifa
xiv) Wazazi wa fao wanampleka kwa masomo ya juu ng'ambo kwa hela zilizonuiwa kuwasaidia watoto maskini
xv) Afisa wa kilimo anamringa dadake Fao
xvi) Serikali inakosa kuwajibikia mashujaa wa kitaifa kama chechwe makweche na matuko weye
xvii) Wananchi kutiwa nguvuni bila sababu yoyote na hata hawapi nafasi kujieleza wala kujitetea k.m. Amani na Imani
xviii) Wauguzi katika zahanati ya Nasaba Bora kukataa kuwatibu wagonjwa mf uhuru
xix) Nasaba Bora anakataa kuwachanja mbwa wake kwa mujibu wa sheria
xx) Majisifu anaba mswada wa Amani badala ya kumsaidia aweze kumchapisha kama kitabu chake
xxi) Mtemi Nasaba Bora kutoa hongo ili madhubuti apate ajira katika jeshi la wanabora
xxii) Mtemi kutumia pesa za kujenga hospitali kuchenga zahanati

zozote 20 x 1= alama 20

4.
a) Msemaji – Tunu
Msemaji – Majoka
Mahali – ofisini mwa Majoka
Sababu – Tunu na Sudi wamemtembelea Majoka ofisini kumweleza kuhusu vijana waliouawa katika Majoka and Makoja Company

b) Balagha – Ukichinja watoto wa wenzio usiulizwe?"
Taswira – ukichinja watoto wa wenzio 2 x 2 =alama 4

c) Tunu alimwita Majoka muuaji baada ya kukataa pendekezo lake kuwa amwoe Ngao Tunu
Tunu alimwambia kuwa hataki kuolewa na wahuni, pia kuwa ngao junior ni gume gume

2 x 2=alama 4

d) i) Majoka anawachinja watoto kwa kufunga soko la chapakazi. Watoto wa Sudi wanakosa kupata kitu cha kutia tumboni
ii) Majoka anawachinja watoto kwa kuwapa elimu duni. Ashua anasema elimu wanayopewa hawafai hawafuzu na wanaishia kuwa wajinga
iii) Utawala wa Majoka unawaua vijana watano waliokuwa wakiandamana
iv) Vijana wengine Sagamoyo wanatumiwa kuendeleza udhalimu kupitia vitendo vya kihuni wahuni wanamwumiza Tunu.
v) Hakuna huduma za afya – wauguzi wanaandamana
vi) Soko la Chapakazi kufungwa kinasababisha adha ya maisha kwa sababu watu wanashindwa kujikimu
vii) Kuna kiwanda kubumbwa cha dawa za kulevya barani Afrika. Dawa hizo zinawaangamiza vyana wa Sagamoyo
viii) Kitendo cha kuruhusu pombe haramu mangweni ni njia nyingine ya kuangamiza watu. Uteri 8 x 1 = alama 8

5. Sumu ya nyoka husababisha madhara mengi kwa mhusika/kiwemo kuua. Kuna mambo mengi yanayodhuru au kuwaua wananchi katika utawala wa Majoka

i) Unyakuzi wa ardhi – Majoka na mshairi wajifurahia eneo la soko la chapakazi ili ajenge hoteli ya kifahari
ii) Kuamrisha askari kutawanya waandamanaji na kusababisha kifo cha vijana watatu

iii) Vitisho – wanaharakati wanaopinga utawala wa Majoka wanatishwa. Kuna vikaratasi vinavyorushwa katika makazi yao ili wahame (siti anamweleza mamake Tunu)
iv) Kuangamiza wapinzani wake – Jabali aliuawa kwa njama za Majoka na chama chake kikasambaratika
v) Ukosefu wa utu. Majoka hathamani utu/uhai wa mtu. Majoka anaamrisha watu wapigwe risasi bila kujali
vi) Tengatawala – uhasama unapandwa na viongozi ili kuwagaza wananchi mf. Sudi ana uhasama na Boza sababu wako katika mirengo tofauti ya kisiasa
vii) Kuzorota kwa maendeleo. Jimbo la Sagamoyo limetimiza miaka sitini ya uhuru lakini bado liko nyuma kimaendeleo
viii) Rushwa– Mamapima anatoa hongo ya uroda kwa Ngurumo ili apate mradi wa kuoka keki ya uhuru
ix) Elimu mbovu – elimu inayotolewa katika shule za kifahari inawalemeza vijana badala ya kuwandaa wawe wazalendo majoka and majoka academy
x) Utawala wa kiimla – Majoka anataka aendelee kutawala ingawa urubani umemshinda na amekwisha zorotesha nchi
xi) Matabaka – Sumu ya nyoka iliyozagaa katika jimbo la Sagamoyo imesababisha kuwapo kwa matabaka
mabwenyeye – Majoka, kenga – maskini – wananchi
xii) Uvivu na ubwete – Majoka ni kiongozi ambaye hajali umuhimu wa kazi. Anatenga mwezi mmoja ya kupumzika katika kuadhimisha miaka 60 ya uhuru
xiii) Ukimtamba – Majoka ana rasilimali nyingi na miradi mingi mikubwa. Anamiliki Majoka and Majoka Company, Majoka and Majoka modern resort
xiv) Ukoloni mamboleo. Jimbo la Sagamoyo linaongozwa kwa mikono ambayo halipwa kwa muda mrefu. Halipwa kwa vizazi vya sasa na hata vyavyo
xv) Ufujaji wa fedha za umma. "Mikopo iliyochukuliwa haikatumika vizuri. Kenga anamweleza Sudi kuwa akikubali kuchonga kinyago cha marara bin Ngao angepata fedha za kubadilisha maisha yake
xvi) Kuwafunga raia bila sababu – mf Ashua kutiwa mbarani ili iwe funzo kwa Sudi
xvi) Kupanga njama ya kumwua Tunu
xvii) Kufunga soko la chapakazi ambayo ni tehemeo kwa raia wa sokomoko
xviii) Majoka anamwambia kenga lazima chatu mmoja atolewe kafara (auawe)
ixx) Anapanga kutumia mamlaka kuzima uchunguzi wa Tunu kuhusu kifo cha jabali
xx) Anafuja pesa za kusafisha soko la chapakazi
xxi) Anatumia mamlaka yake kudhibiti vyombo vya habari

**FASIHI SIMULIZI**

6.

a) Miviga – Ni sherehe za kitamaduni ambazo zinafuata utaratibu Fulani wa kisanaa za maonyesho

Mighani – masimulizi kuhusu mashujaa

Visasili – hueleza chimbuko au kitovu cha jamii 4 x 2 = alama 8

Ngano ni masimulizi au hadithi za kimapokeo zitumiazo wahusika wanyama au miti

b) I Mcheshi – awasilishe kwa njia inayochangamsha wasikilizajhi

Aelewe hadhira ili awasilishe kwa njia ipasavyo

Afahamu lugha ya hadhira yake

Awe jasiri – asiogope kuwasisha mbele ya hadhira

Awe mbunifu–kuumba hadithi upya

Awe na uwezo wa kufaragha ili kuvutia hadhira

Awe na kumbukumbu nzuri

Aelewe utamaduni wa jamii

za kwanza 4 x 1= alama 4

ii) Ngomezi ni sanaa ya ngoma

ni maonyesho ya ngoma na ala zingine za kimuziki bila kutumia maneno

1 x 2 = alama 2

iii) Huwa na mdundo wa ngoma wa kipekee

Mdundo wa ngoma huwa na ujumbe tofauti

Kuwepo kwa ala nyingine za muziki

Ngomezi hutegemea mapigo

Huwa na fundi wa kupiga ngoma

Hueleweka na jamii husika pekee 6 x 1 = alama 6

7.

a) Hadhira – fanani anaweza kubadilisha mtindo wake wa utambaji kutegemea hadhira

Wakati - Msamiati unafaa wakati wa usimulizi lazima utumike nahivyo kubadilisha fasihi simulizi

Fanani - kila fanani ana njia yake ya uwasilishaji

Teknolojia - mambo ya kiasi yanabadilishwa na kuongezewa pia kulingana na teknolojia

Mazingira –watu wamehama na hakuna pahali pa uwasilishaji maalum

Video - fasihi simulizi inarekodiwa katika kanda na uwasilishaji wake ni tofauti na farani

Wakati wa usimulizi - uhahisia unakosekana kwa sababu fasihi simulizi inasimuliwa hata mchana darasani au kumbinu

Maandishi - Fasihi simulizi imehifadhiwa katika maandishi na hivyo si simulizi

Mkengeuko –utamaduni hautaminiwa tena kuishia kuleta mabadiliko katika fasihi Simulizi

Kuingiliana kwa tamaduni – mafanani wanachanganya hadithi za tamaduni tofauti ili kuipa fasihi simulizi uhalisia kwa wote

Uhamaji na uhamiaji- katika harakati hizi mengine yana sahaulika na inabida kubuni mapya

Ukosefu wa utafiti – watu wanajijazia kile wasichokijua na kuishia kubadilisha mambo 10 x 1 = alama 10

b) Kuelimisha – kuhusu mambo tofauti tofauti k.m malezi
Hubadilisha – hulengwa kumrekebisha ambaye amepotoka
Huonyesha mtamazo wa jamii kuhusu swala tofauti k.m. uzembe
Huutambulisha jamii – husahau shughuli k.m. kilimo
Huongeza ladha katika lugha huipamba na kuyafanya mazumgumzo yavutie
Huburudisha – hutoa namna ya burudika kwa anayeambiwa na anayezitumia pia
Hurithisha utamaduni – hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine
Hufariji huweza kuambiwa hakuna marefu yasiyokuwa na ncha
Hukejeli – huweza kukefeli tabia hasi – uzembe
Hukuza lugha - -zimesheneni tamathali nyingi za lugha 10 x 1 = alama 10

8.
a) Msemaji – Safia
Msemewa – Bi Hamida Mamake
Mahali – walikuwa nyumbani
Sababu – Bi Hamida alitaka kujua ni kwa nini safia amekosa uchangamfu siku za hivi majuzi. Pia alitaka kujua ni kwa nini alikuwa anatapikatapika
4 x 1= alama 4

b) Bi Hamida alikuwa na wasiwasi kuwa safia huenda alikuwa mjamzito
Matokeo ya kujihusisha kimapenzi na mwanamume 2 x 1=alama 2

c) Mzungumzaji ni safia (taja mzungumzaji kwanza)

i) Mjanja – Anatumia hila na ulaghai kuwaadaa wazazi wake
ii) Mwenye hasira – Bi Hamida anapomdadisi kuhusu hali yake ya kutapika, anapandisha hasira
iii) Katili/muuaji – Anatoa mimba na kukidhulumu kiumbe kisicho na hatia
v) Msaliti – Anawasaliti wazazi wake ambao walijua ni mwaminifu sana na kumpa uhuru wa kudurusu na rafiki yake
vi) Msiri – Anamficha rafiki wake wa kiume kwa kujivisha vazi la kike (buibvui) hadi miguuni

vii) Ana bidi ya mchwa – safia alisoma kwa bidi na daima aliongoza darasani
viii) Mnafiki – anajifanya yeye ni wa dini
ix) Mwerevu – katika kila mtihani, safia aliibuka wa kwanza kabisa katika darasa
8 x 1 = alama 8

Umuhimu wa safia
Yeye ni kielelezo cha vijana wajanja wenye hila, wanaowadanganya wazazi ili

Kupitia kwa huyu mhusika, tunajua kuwa hila na uwongo vina mwisho wake. Mara nyingi huwa ni mwisho mbaya

Safia ametumiwa kuonyesha changamoto za malezi ya watoto

Ametumiwa kuonyesha madhara ya kuavya mimba 3 x 2=alama 6